

Sema Maoni Yako! Utafiti wa mzazi na mlezi juu ya elimu ya idhini – wazi sasa

Idhini ni kusema ndio kwa kitu kutokea au kukubali kufanya jambo kwa huru, bila hofu, nguvu au kusukumwa.

Wanafunzi wa zamani na wa sasa kote jimboni wanataka elimu bora za idhini.

Ombi la hivi karibuni la mwanafunzi wa zamani wa Sydney yani Chanel Contos lilisababisha maelfu ya vijana kushiriki hadithi zao za kushahidi au kupitia unyanyasaji, matumizi mabaya na ukatili wa kingono kati ya vijana. Hii ilisababisha wito kwa elimu ya mapema na bora ya idhini kwa wanafunzi.

Idara ya Elimu ya NSW (Department) imeahadi kushughulikia pamoja na wazazi kuboresha elimu ya idhini.

Tutapenda kusikia maoni yako. Tafadhali utuambie unachofikiri kwa kukamilisha utafiti mfupi unaofuata wa wazazi bila kujulikana: [Consent education survey link](#)

Utafiti huu unapatikana katika Kiingereza na lugha 10 nyingine na utachukua kidogo kuliko dakika 10 kukamilisha. Utasaidia Department kuelewa wazazi na walezi wanachojua juu ya elimu ya idhini katika shule siku hizi, na aina gani ya nyenzo itakayowasaidia kuongea kuhusu idhini na watoto na vijana wao nyumbani.

Matokeo ya jumla yatashirikiwa kwenye tovuti ifuatayo ya Idara ya Elimu NSW baadaye mwaka huu: [Consent education website](#)

Department inataka kusikia kutoka wazazi na walezi wa wanafunzi wa shule za serikali za NSW kutoka jamii zote. Pamoja, tunaweza kuwasaidia watoto na vijana wetu kujenga mahusiano mazuri.

Sema maoni yako kwa kukamilisha utafiti sasa. Nenda kwa [Consent education survey](#)